

Neno la Mchapishaji

Kitabu kilichoko mikononi mwako ni tarjuma ya kitabu cha Kiingereza kiitwacho, Anecdotes. Sisi tumekiita, Visa vya Kweli. Kitabu hiki kimeandikwa na Sayyid Ali Akbar Sadaaqat.

Kitabu cha Visa vya Kweli kimekusanya simulizi za visa vya kweli vilivyosimuliwa katika Qur'ani Tukufu, hadithi na riwaya na vyanzo vingine sahihi. Kwa kweli, visa hivi hufundisha maadili mema kwa wanadamu, hivyo, kitabu hiki tunaweza kukiita kuwa ni cha maadili kwa kuwa visa vilivyoelezewa humu ni vya kimaadili.

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu ambapo kuna mmomonyoko mkubwa wa maadili. Kitabu hiki kitawafaa sana vijana walioko mashuleni na vyuoni, halikadhalika watu wa wazima.

Taasisi yetu ya Al-Itrah Foundation imeamua kukichapisha kwa lugha ya Kiswahili kwa malengo yaleyale ya kuwahudumia wasomaji wetu wazungumzao Kiswahili ili wapate kuongeza elimu yao ya dini na ya kijamii kwa ujumla.

Tunawashukuru ndugu zetu, Dr. M. S. Kanju na Mwl. Aziz Njozi kwa kukubali jukumu hili la kukitarjumi kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake.

Mchapishaji:

Al-Itrah Foundation

S. L. P. 1970

Dar-es-Salaam,

Tanzania.